JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE – NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI MAKETE WASICHANA

S.L.P 36, MAKETE **SIMU: 0766252580**

……..……..……..

C. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inavyotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

SHERIA ZA SHULE

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughili za shule na zingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kutunza heshima na jina la shule pamoja na kuifanya shule mahali pa amani.
(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(j) Kutunza mali za umma.

D. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE

(a) Wizi.
(b) Uasherati na ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
(e) Kuharibu maksudi mali ya umma.
(f) Kudharau bendera ya Taifa.
(g) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba.
(h) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(i) Kukataa adhabu kwa maksudi.
(j) Kuwa na simu ya mkononi

E. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

(a) Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni (imeambatanishwa)
(b) Form ya mzazi kushiriki kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule. (imeambatanishwa)

NB: Kama mwanao ana BIMA YA AFYA ni vema akafika nayo.

F. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

1. Mwanao aje na mafaili mawili, moja kwa ajili yake na jingine la kuweka kumbukumbu zake za kitaaluma. Pia aje na dictionary/kamusi
2. Mzazi unashauriwa kumununulia mwanao kitabu kimojawapo kati ya hivi. Hawa the Bus driver, Mabala the farner au The Magic Garden.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MAKETE

……
SAYUNI EMBASY SANGA
MKUU WA SHULE

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

FOMU YA MZAZI NA MWANAFUNZI KUKUBALIANA NA KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Kwa mzazi/mlezi wa ……...

1. Napenda kukupongeza kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza hapa shule ya sekindari wasichana Makete. Ni mategemeo ya shule kuwa utajitahidi kwa uwezo wako wote kumsaidia ili aweze kusoma bila matatizo (kwa kutimiza mahitaji yote ya muhimu kwa wakati).
2. Ili mtoto wako aweze kufanikiwa ni muhimu awepo shuleni muda wote wa masomo. Hivyo huna budi kumsaidia ili vikwazo visivyo vya lazima visiwepo.
3. MAKUBALIANO YA TAALUMA YA MWANAFUNZI

   Mwanafunzi yeyote anayejiunga na shule hii atatakiwa kuwa na ufaulu wa divisheni ONE, TWO NA THREE TU katika mitihani yote. Kwa mwanafunzi atakayefeli kwa kupata divisheni FOUR AU ZERO mzazi atatakiwa kumtafutia shule nyingine mwanae. Nakusihi mzazi anza kuongea na mtoto kulifahamu hilo ili akifika shule akazane kusoma ili asipoteze nafasi hii.
4. Tafadhali jaza fomu iliyoambatanishwa kama inavyojieleza.

A. AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi ……...
Mzazi/Mlezi wa (jina la mtoto) ……..
Ninakubali aingie shule ya sekondari ya wasichana Makete na ninaahidi kumtimizia mahitaji yote yaliyoagizwa.
Pia naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule na kumtunza ki – Tanzania (awapo shuleni na likizo) mpaka atakapo maliza masomo yake. Na kama kuna mabadiliko nitautaarifu uongozi wa shule.
Anuani yangu ya kudumu: Kijiji …….. Kata ……
Simu: ya mzazi/mlezi ……
Sahihi …….. Tarehe ……..

B. AHADI YA MWANAFUNZI:

Mimi …… nakubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari ya wasichana Makete. Naahidi kuwa nitazitii sheria zote za shule na kufuata maelekezo na maagizo nitakayopewa na Mkuu wa shule, wafanyakazi na viongozi wote wa serikali ya wanafunzi. Nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo,na kusoma kwa bidii, elimu ya kujitegemea, michezo na kutunza usafi wa mazingira ya shule kwa muda wote nitakao kuwa sekondari ya wasichana Makete.
Shule niliyosoma ni …… Namba ya mtihani ni …….……
Sahihi ……. Tarehe ……..

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

SEHEMU YA MGANGA

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
MAKETE GIRLS SECONDARY SCHOOL
(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)

This form must be completed by a Government Medical Officer.
Name of student ……..
Age …….. Sex ……

The above named student has been examined in respect of:

a) PREGNANT TEST ……
b) STOOL ……
c) URINE ……
d) CHEST ……
e) BLOOD ……
f) EYES ……
g) EARS ……
h) HEAMAGLOBIN ……
i) P. V. BLEEDING ……
j) ASTHMA ……
k) SKIN DESTASL ……
l) LEPROSY ……
m) ETHEPSY ……
n) ANY DETORMITY ……
o) T.B ……
p) NEUROSIS ……
q) VENEREAL DISEASE ……
r) OTHER FINDINGS ……
……
……
……
……

I am satisfied that the above student is fit/not fit for pursuing secondary studies at MAKETE GIRLS SECONDARY SCHOOL.

……. ……
SIGNATURE DATE

……. ……
DESIGNATION AND OFFICIAL STAMP *STATION*

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL